# Paradigms High School

"Africa centre for Educational Excellence"

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**


**Tarehe: _____**

**MZAZI/MLEZI WA: _____**

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA ..... MWAKA .....**

1. Nafurahi kukujulisha kuwa mtoto wako _____ amechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha ..... mwaka ....., mchepuo wa .....

2. **SHULE ILIKO:**
   SHule za Paradigms ziko eneo la Bunyokwa, kata ya Kimara km 3.5 kusini mwa barabara ya morogoro, wilaya ya Kinondoni, Dar Es Salaam, unaweza kuingilia Kimara mwisho au Suca. Ni shule ya Bweni na kutwa na ya mchanganyiko wa wasichana na wavulana.

3. **KUFUNGUA SHULE:**
   Shule itafunguliwa rasmi tarehe 3/1/2009. Mwanafunzi anatakiwa awe ameripoti tarehe 10/1/2009. Mwanfunzi ambaye atakuwa hajaripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua shule hatapokelewa na nafasi yake itatolewa kwa mtu mwingine.

4. **MASOMO:**
   **A. HIGH SCHOOL**
   Michepuo iliyopo hapa shuleni ni
   HGL-History, Geography, English General studies
   HGK-History, Geography, Kiswahili General studies
   HKL – History, Kiswahili, English Language, General Studies
   HGE – History, Geography, Economics, Basic applied mathematics & General Studies
   EGM – Economics, Geography, Advanced Mathematics, General Studies
   PCM – Physics, Chemistry, Advanced Mathematics, General Studies
   PCB – Physics, Chemistry, Biology and General Studies
   **B. SECONDARY SCHOOL .**

Masomo yanayofundishwa hapa shuleni ni Hesabu, Fizikia, Biologia, Kemia, Kiswahili, Kiingereza, Jiografia, Historia, Uhasibu, Biashara na Uraia.

**5. A) 1) LUGHA:**
Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza na ndiyo lugha ya mawasiliano mwanafunzi awapo shuleni.

**2) KARO:**
Gharama za karo na mchanganuo vimeambatanishwa nyuma.

**HATUPOKEI CHEQUE:**

Bank Pay in Slip iletwe shuleni na mwanafunzi atapewa risiti. Andika jina kamili la mwanafunzi kwenye fomu ya kuwekea hela wakati unapopeleka hela bank.

**KUMBUKA:**
1. Shule haitawajibika kulipa au kurudisha sehemu yoyote ya malipo ya karo baada ya mwanafunzi kusajiliwa rasmi kwa sababu yoyote ile.
2. ADA ya shule ilipiwe Bank yoyote ya CRDB – A/C No. 1009183700 kwa jina la Paradigms Secondary School.

**B) VITABU**
Unatakiwa umnunulie mwanao vitabu vifuatavyo;

**(a) SECONDARY**
a) Secondary basic mathematics
b) English for secondary schools
c) Book keeping for secondary schools
Vitabu hivi vinapatikana katika duka la shule kama hutavipata eneo jingine.

**(b) A'LEVEL**
(mahitaji yameambatanishwa)

**MAHITAJI MENGINE:**

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**

Malipo ya ziada yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) Mitihani ya majaribio (Mock Examinations) Tshs 10,000/= (Kiwango hiki kinaweza kubadilika kila mwaka).

(b) Alete Tshs 8,000/= kwa ajili ya T-shirt zitakazovaliwa siku ya Jumatano na Ijumaa.

**6. BWENI:**

(a) Wanafunzi wote wanaoomba nafasi ya kuishi bwenini wajaze fomu za maombi ya Bweni (zimeambatanishwa).

Zirudishwe zikiwa zimejazwa kwa ufasaha.

**7. SARE:**

**(a) WAVULANA: KIDATO CHA KWANZA – NNE**

(i) Suruali ya rangi ya bluu, shati jeupe la mikono mifupi lenye nembo ya shule kwenye mfuko, tai ya rangi ya suruali na hivi vyote vinatolewa shuleni.

(ii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa kwa kamba(gidam) visivyo na mapambo ya aina yoyote, na vyenye soli fupi. (Mabuti hayaruhusiwi)

(iii) Soksi nyeusi

**(b) WASICHANA:**

(i) Sketi ya rangi ya bluu ambayo urefu wake uwe Inchi moja chini ya goti, yenye mshono wa **V,** shati nyeupe mkono mfupi lenye nembo ya shule kwenye mfuko na skafu ya rangi ya sketi hivi vyote vinapatikana shuleni.

(ii) Viatu vya ngozi nyeusi visivyo na mapambo yoyote, visigino vifupi

(iii) Soski rangi **nyeupe** zisizo na mapambo yoyote au matundu.

**8. SARE: KIDATO CHA 5 NA 6.**

**A) WAVULANA:**

i) Suruali ya rangi ya kijani, shati jeupe la mikono mirefu lenye nembo ya shule kwenye mifuko na tai rangi ya suruali.

ii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa kwa kamba (gidam) visivyo na mapambo ya aina yeyote na vyenye soli fupi.

**B) WASICHANA**

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**

i) Sketi ya rangi ya kijani yenye mshono wa **V** ambayo urefu wake uwe inch 1 chini ya goti, shati jeupe la mikono mirefu lenye nembo ya shule kwenye mifuko na skafu rangi ya sketi hivi vinapatikana shuleni.

ii) Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na mapambo ya aina yeyote na vyenye soli fupi.

iii) Soksi rangi nyeupe zisizo na mapambo yeyote au matundu.

Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuja shuleni na vitu vya thamani kama simu za mikononi, Radio, Walkman, Kamera, Mikufu ya aina yoyote, pesa nyingi zinazozidi 50,000/= utawala hufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Ukipatikana navyo utachukuliwa, utaadhibiwa na hutarudishiwa.

**KARIBU PARADIGMS HIGH SCHOOL**

_____

**MKUU WA SHULE**

Mwaka: 2009

# Paradigms High School

"Africa centre for Educational Excellence"

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**


Kumb No. PHS/UTH/1/01

## HATI YA UTHIBITISHO

**MWANAFUNZI:**

Mimi.....
Nathibitisha kuwa nimesoma na kuelewa Kanuni za shule na naahidi kuwa nitazifuata wakati wote nitakaokuwepo shuleni.

Sahihi: ..... Tarehe: .....

**MZAZI/MLEZI:**

\
Mimi.....Mzazi/Mlezi wa .....
Ninathibitisha kuwa nimezisoma na kuzielewa vizuri kanuni za shule; ninaahidi kuwa nitashirikiana na shule ili mwanangu aweze kuzifuata kanuni hizi.

Sahihi: ..... Tarehe: .....

Mahali unapoishi: -

Mkoa:..... Wilaya: ..... Mtaa: .....

Anwani:.....

.....

.....

Simu:- Nyumbani:..... Mkononi .....

Kazini: .....

E-mail / Barua pepe .....

**NB:** Rudisha hati hii baada ya kusoma kanuni na kuzielewa na kusaini.

**MKUU WA SHULE**

## KANUNI ZA SHULE

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**

## 1. WAJIBU WA MWANAFUNZI:

Mwanafunzi anapokuwa hapa shuleni anapaswa azingatie yafuatayo: -

(a) Kuingia na kukaa kimya darasani
(b) Kuwa msafi wakati wote na kufanya maeneo ya shule kuwa safi
(c) Kuwa mtiifu mbele ya walimu, wafanyakazi wa shule, viongozi wa wanafunzi na wanafunzi wenzake.
(d) Kutunza mali yake binafsi na mali za shule.
(e) Kuepukana na utani kati ya Mwanafunzi na Mwanafunzi kupita kiasi.
(f) Kutoingia katika ofisi za walimu, iwapo walimu hawamo ofisini.
(g) Kutoa taarifa kwa mwalimu wa darasa, zamu, ofisi ya nidhamu, taaluma au Ofisi ya Mkuu wa shule juu ya tukio ambalo sio la kawaida
(h) Kutokuzurura nje ya darasa wakati wa masomo.
(i) Kutokutoka nje ya shule bila ruhusa kutoka kwa Mwalimu wa zamu.
(j) Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara, kupaka mafuta ya kuchubua ngozi, kuweka/kupaka nywele dawa, kupaka kucha rangi, kuvaa pete, hereni au mkufu, kuvaa vazi la kubana (skin tight au kujirembesha kwa aina yeyote ile) Nywele zake zitakuwa ziwe na urefu wa robo nchi au zisukwe (twende kilioni) na safi wakati wote atakaokuwepo hapa shuleni.
(k) Lazima Mwanafunzi awe kwenye sare ya shule wakati wote katika mazingira ya shule. Nikosa kuingia darasani bila sare kwa sababu yoyote ile.
(l) Ndugu, marafiki au jamaa za wanafunzi hawaruhusiwi kuwatembelea na kuongea na mwanafunzi bila idhini ya mwalimu Mkuu / wa zamu.

**Ni marufuku kwa mwanafunzi: -**

(a) Kuiba mali ya shule au mali ya mwanafunzi mwenzake.
(b) Kupata mimba au kumpa mimba mwanafunzi mwenzake
(c) Kutoroka shuleni
(d) Kuvuta sigara, bangi, kunywa pombe au madawa ya kulevya

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**

(e) Kutukana, kupigana na mwanafunzi mwenzake, au kumpiga mwalimu / mfanyakazi yeyote wa shule.
(f) Kutoka nje ya shule bila idhini ya mwalimu
(g) Kufanya au kushiriki katika udanganyifu wakati wa mitihani
(h) Kuharibu au kuvunja mali ya shule kwa makusudi au kushirikiana na watu wengine katika kufanya uhalifu wa mali za shule
(i) Kutokufanya mitihani (mitatu) ya majaribio bila sababu inayotambuliwa na mwalimu wa darasa
(j) Kuwa na urafiki usio wa kimasomo kati ya mwanafunzi msichana na mvulana.
(k) Kutotii amri zinginezo za shule

Endapo mwanafunzi atafanya moja kati ya makosa yaliyotajwa juu, au Lingine linalofanana au lenye uzito sawa au zaidi ya hayo, anastahili **ADHABU** kali, mojawapo ikiwa **KUFUKUZWA** shule moja kwa moja

**FOMU YA MAOMBI YA BWENINI**

(Ijazwe na irudishwe kabla ya tarehe …….)

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**

## SEHEMU YA 1

1. (a) Jina kamili la mwanafunzi .....
   (b) Tarehe ya kuzaliwa .....
   (c) Kidato cha .....
   (d) Shule aliyotoka ..... Mkoa .....

2. (a) Jina kamili la mzazi/mlezi .....
   (b) Mahali anapoishi ..... Mtaa.....

3. (a) Anwani kamili ya Mzazi / Mlezi.....
   (b) Simu (i) Nyumbani ..... (ii) Ofisini .....
   (iii) Mkononi.....
   (iv) Barua pepe .....

4. Je, mwanafunzi ana matatizo ya kiafya? NDIYO/ HAPANA
   Kama jibu NDIYO yataje

.....

.....

.....

.....

**(Ambatanisha vyeti vya daktari)**

5. Orodhesha majina MATATU ya Ndugu wa karibu ambao wataruhusiwa kuja kumwona mwanao kwa niaba yako (wawe na vitambulisho)

| | **JINA** | **UHUSIANO** | **SAHIHI** |
|---|---|---|---|
| 1. | _____ | _____ | _____ |
| 2. | _____ | _____ | _____ |
| 3. | _____ | _____ | _____ |

## GHARAMA ZA SHULE

Gharama za mwanzo za kujiunga na shule zinazolipwa mara moja

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**

Mwanafunzi anapoanza shule ni T.shs. 200,000/= mchanganuo umeambatanishwa.

Ada ya shule (Kutwa na Bweni) ni kama inavyofafanuliwa hapa chini

**A. Mwanafunzi wa Sekondari**

| | KUTWA | BWENINI |
|---|---|---|
| **Ada** | 250,000 x 3 = 750,000.00 | 400,000 x 3 = 1,200,000.00 |

**B. High School**

**1. Mwanafunzi wa ARTS / COMMERCE**

| | KUTWA | BWENINI |
|---|---|---|
| **Ada** | 275,000 x 3 = 825,000.00 | 425,000 x 3 = 1,275,000.00 |

**2. Mwanafunzi wa SCIENCE**

| | KUTWA | BWENINI |
|---|---|---|
| **Ada** | 325,000 x 3 = 975,000.00 | 450,000 x 3 = 1,350,000.00 |

**KARIBU PARADIGMS HIGH SCHOOL**

## SEHEMU YA II

**MAHITAJI MUHIMU – WANAFUNZI WA BWENI**

Kila mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa vifuatavyo; -

1. (i) Mashuka manne (Bed sheets) rangi ya blue, chandarua kimoja kiwe cha square na ngao, mto mmoja na foronya mbili. Vyote vinapatikana katika duka la shule.

2. Sahani, kikombe cha chai kikubwa na kijiko. Vinapatikana duka la shule.

3. Taulo, mswaki, dawa ya meno, sabuni za kufulia na kuogea na mafuta ya ngozi.

4. Ndoo moja (lita 20)

5. Wasichana Sketi / Wavulana kaptula mbili za rangi ya light green sampuli ya kitambaa itatolewa shuleni. Hizi zitavaliwa baada ya masomo na siku ya Jumamosi na Jumapili (za kushindia) Zinapatikana shuleni kwa 10,000 kwa moja.

6. Fulana mbili za rangi ya kijivu hizi zinapatikana shuleni kwa Tshs. 5,000 /= kila moja (za kushindia)

7. Fedha za matumizi (pocket money) zisizidi Tshs. 50,000/=

**ONYO:** Usije na nguo za nyumbani, zaidi ya khanga 2 kama wewe ni msichana.

## SEHEMU YA III

## MASHARTI YA KUKAA BW ENINI

1. Wanafunzi wote watajiandikisha katika kitabu maalumu kwa Mkuu wa Shule siku wanaporipoti na kulipa gharama za Bweni. Awe amesoma na kuzikubali sheria na kanuni za shule.

2. Usafi wa ndani na nje ya Bweni utafanywa na wanafunzi wenyewe. Usimamizi na ratiba ya usafi itapangwa na viongozi wa Bweni pamoja na Matron wao.

Kimara; Bonyokwa P.O. Box 78703, Tel +255 732 926349, Mobile: 715 263999, 715 758093
**E-mail: paradigmsltd@yahoo.co.uk, Website: www.paradigms.co.tz**

3. Ni marufuku kupika kitu chochote ndani ya Bweni.

4. Ni marufuku kuingia na vyakula vyovyote ndani ya Bweni, vyakula vitaliwa D/Hall tu.
5. Ni marufuku kupiga makelele, kutumia lugha chafu, kupigana n.k katika bweni. Wanafunzi watakaopatikana na makosa haya watakuwa wamepoteza sifa za kuishi Bwenini na malipo hayatarudishwa.

6. Hairuhusiwi kuwa na Radio, TV, Camera, Simu ya mkononi katika Bweni, Vikikamatwa havitarudishwa.

7. (a) Wanafunzi wasio wakazi wa Bwenini hawaruhusiwi kuingia ndani ya Bweni
   (b) Wageni WOTE hata ndugu wa wanafunzi **HAWARUHUSIWI** kuingia ndani ya mabweni. Yeyote atakayevunja amri hii atakuwa amepoteza sifa za kuishi Bwenini hivyo atafukuzwa mara moja.

8. Kila mwanafunzi atunze mali yake / wenzake kwa uaminifu, wanafunzi wezi wa vifaa vya wengine hawataruhusiwa kuishi Bwenini. Watafukuzwa mara moja.

9. Kila Mwanafunzi lazima awe msafi wa mwili, nguo na chumba chake.

10. Wanafunzi watakaobainika kutolala bwenini au kutoroka na kurudi bila idhini ya MATRON watakuwa wamepoteza sifa ya kushi Bwenini, hivyo wataondolewa.

11. Mwanafunzi atakayeingiza mwanafunzi mwenzake, awe msichana au mvulana, au mgeni yeyote Bwenini atafukuzwa kukaa Bwenini.

**12. KUMBUKA: Wizi, uasherati, ulevi, kupigana, utumiaji wa madawa ya kulevya au sigara, kupata / kutoa mimba ni makosa ambayo UTAFUKUZWA BWENINI na shuleni mara moja.**

**MKUU WA SHULE**

**SEHEMU YA IV**

Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi baada ya kusoma na kukubaliana na Masharti yaliyomo humu.

Mimi _____ mzazi/mlezi wa mtajwa juu naahidi kumlipia mwanafunzi mtajwa gharama zilizotajwa na nakubaliana na masharti yote yaliyotajwa.

Sahihi: ..... Tarehe: .....